# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# SERA YA TAIFA YA WAZEE

**WIZARA YA KAZI,**
**MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO**

**SEPTEMBA, 2003**

## YALIYOMO

### SURA YA KWANZA

UKURASA

**1.0. UTANGULIZI........................................................................ 1**
1.1 Dhana na maana ya uzee ........................................................ 2
1.2. Hali ya wazee nchini .................................................................. 3
1.2.1 Mmomonyoko wa maisha ya kijadi ............................................ 3
1.2.2. Matunzo duni ........................................................................... 4
1.2.3 Umaskini ................................................................................... 4
1.2.4 Magonjwa .................................................................................. 4
1.2.5 Wanawake wazee na mila zilizopitwa na wakati.............................. 4
1.2.6 Wanawake wazee wenye ulemavu ............................................ 5
1.2.7 Sheria zisizolinda na kuendeleza wazee ..................................... 5
1.3 Sababu za kuwa na Sera ya Wazee. ........................................... 5

### SURA YA PILI

**2.0. MWELEKEO WA SERA................................................... 7**
2.1. Mwelekeo ................................................................................... 7
2.2. Madhumuni ya jumla................................................................... 7
2.3. Madhumuni mahususi.................................................................. 7

### SURA YA TATU

**3.0 MATAMKO YA SERA........................................................ 9**
3.1. Huduma za afya ......................................................................... 9
3.2. Matunzo ya wazee ..................................................................... 10
3.3. Ushirikishwaji wa wazee ............................................................ 11
3.4. Mfuko wa wazee ....................................................................... 11
3.5. Uzalishaji mali ........................................................................... 11
3.6. Hifadhi ya Jamii ......................................................................... 12
3.7. Mahitaji ya msingi ya maisha uzeeni............................................ 12
3.8. Elimu ......................................................................................... 13
3.9. Wanawake wazee na mila zilizopitwa na wakati............................ 13

3.10. Wanawake wazee wenye ulemavu .............................................. 14
3.11. Sheria zisizolinda na kuendeleza wazee ...................................... 14
3.12. Malezi na maandalizi ya vijana kuelekea uzeeni ................................ 14
3.13. Vyama vya kuhudumia wazee ..................................................... 15
3.14. Mabaraza ya Wazee.................................................................. 16
3.15. Ushirikishwaji wa Wadau........................................................... 16

**SURA YA NNE**

**4.0. MGAWANYO WA MAJUKUMU........................................ 17**
4.1. Serikali Kuu ............................................................................. 17
4.2. Serikali za Mitaa ........................................................................ 17
4.3. Familia/vijiji.............................................................................. 18
4.4. Wakala za Hiari .......................................................................... 18

# DIBAJI

Tangu nchi yetu ilipopata Uhuru wake mwaka 1961 haja ya kuwa na mwongozo wa kitaifa kama dira ya kuelekeza huduma kwa Wazee ilibainika. Ilidhihirika waziwazi kuwa huduma zilizokuwa zikitolewa kwa wazee zilihitaji kuwekewa malengo na uratibu mzuri ili walengwa waweze kunufaika vizuri na pia kuzingatia matarajio yao.

Mnamo mwaka 1982 Umoja wa Mataifa ulitoa Mpango wa Kimataifa wa utekelezaji ikiwa ni dira ya kimataifa ya utoaji huduma na ushirikishwaji wa wazee katika maendeleo yao na ya jamii kwa ujumla. Mpango huu wa Kimataifa ulifanyiwa mapitio mwaka 2002 kwa lengo la kuainisha matatizo na mahitaji ya wazee katika karne ya 21.

Katika kuadhimisha Mwaka wa Kimataifa wa Wazee (1999) Serikali ilifanya maamuzi ya kuwa na Sera ya Taifa ya Wazee. Maamuzi ya kuwa na Sera ni kielelezo cha dhamira ya Serikali ya kuweka masuala ya wazee katika agenda ya maendeleo ya nchi yetu. Tunatambua kwamba wazee wetu wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwa ni pamoja na umaskini, kutotosheleza kwa huduma za afya, pensheni na kutoshirikishwa katika maamuzi muhimu yanayohusu maendeleo ya nchi yetu. Mmomonyoko wa maadili katika jamii umewaathiri wazee walio wengi. Pamoja na hali hii tunatambua kwamba wazee ni raslimali na nguvu mpya katika maendeleo ya nchi yetu. Kila jitihada itawekwa kuhakikisha kwamba wazee wanatambuliwa na wanapata fursa ya kushiriki katika shughuli za maendeleo ya nchi yetu sambamba na wananchi wengine.

Kuwapo kwa Sera ya Taifa ya Wazee ni hatua ngeni kwa nchi nyingi, Tanzania ikiwa moja wapo. Katika Afrika, Tanzania ni nchi ya pili kuwa na Sera ya aina hii baada ya Mauritius. Endapo kutatokea upunguf katika matamko na utekelezaji wa Sera yenyewe Wizara itakuwa tayari kufanya marekebisho pale yanapohitajika. Wizara inakaribisha maoni/mapendekezo kutoka kwa wote ambao wanahusika na utekelezaji wa Sera hii.

Kwa watumishi wa Wizara, Sera hii nimwongozo katika kuandaa mipango, utekelezaji na tathmini ha utoaji huduma kwa wazee.

Wizara inato shukrani kwa watumishi, wazee wenyewe na taasisi mbalimbali kwa mchango wao katika kufanikisha kuwappo kwa Sera hii. Napenda kutoa shukrani za pekee kwa shirika la Help Age International kwa mchango wao mkubwa katika maandalizi ya Sera hii.

Prof. Juma A. Kapuya (MB)
**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO.**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI.

Suala la uzee na kuzeeka limekuwa lenye umuhimu mkubwa kwa jumuiya ya kimataifa hasa kuhusiana na mitazamo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Taarifa za umoja wa mataifa (1999) zinaonyesha kuwa kumekuwa na ongezeko la idadi ya wazee Duniani. Ongezeko hili linaonekana zaidi katika nchi zinazoendelea ambapo viwango vya ongezeko havilingani na uwezo wa rasilimali zilizopo kuwahudumia katika nyanja za afya, lishe na huduma nyingine za msingi kwa maisha ya binadamu.

Kulingana na taarifa hizo, mwaka 1950, Umoja wa Mataifa ulikadiria kuwepo kwa watu millioni 200 wenye umri wa miaka 60 na zaidi. Mwaka 1975, idadi hiyo iliongezeka na kufikia millioni 350. Idadi hiyo inategemewa kuongezeka na kufikia milioni 625 ifikapo mwaka 2005.

Inatarajiwa pia kuwa ifikapo mwaka 2050, idadi ya wazee, kwa mara ya kwanza katika historia ya binadamu, itaongezeka na kuzidi ile ya watoto/vijana chini ya miaka 24. Idadi hiyo katika bara la Afrika pekee inategemewa kuongezeka kutoka milioni 38 ya sasa na kufikia milioni 212 ifikapo mwaka 2050.

Kuongezeka kwa idadi na asilimia ya watu ni mafanikio kwa kuwa ni kielelezo cha ubora wa maisha unaotokana na kuboreka kwa huduma kama vile za afya na elimu. Hata hivyo ongezeko hilo ni changamoto kwa sababu Serikali inawajibika kuwa na miundo mbinu inayopasika kutoa huduma kwa wazee. Hii ni nafasi muafaka kwa jamii kuongeza kasi ya maendeleo yetu.

Wazee wengi huishi katika umaskini hali ambayo inaleta mashaka makubwa kwao. Kadhalika ukweli kwamba idadi kubwa ya wazee (takribani asilimia 75) wanaishi vijijini na kwamba idadi ya wazee wanawake ni kubwa zaidi kuliko wazee wanaume unaleta changamoto ya ziada. Upo umuhimu mkubwa kwa Serikali,taasisi zake na Wakala za Hiari kuandaa mazingira yanayowatambua wazee na yanayotoa nafasi kwao kushiriki kwa ukamilifu katika maisha ya kila siku ya jamii.

Serikali inatambua kwamba wazee ni rasilimali na hazina kubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Kuwapo kwa taifa la Tanzania ni kielelezo tosha cha mchango mkubwa wa wazee walioutoa katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii.

## 1.1 DHANA NA MAANA YA UZEE.

Uzee na kuzeeka ni dhana inayoelezea hatua ya mwisho ya makuzi ya binadamu kuanzia utoto, ujana hadi kufika uzee. Hapa Tanzania mtu anaitwa mzee kutokana na ama umri mkubwa, majukumu aliyonayo na pia hadhi yake, kwa mfano mkuu mahali pa kazi au katika ukoo. Wazee tulionao aidha walikuwa wanafanya kazi za kuajiriwa au kujiajiri au ni wale walioko vijijini ambao kuzeeka kwao ni matokeo ya kupungukiwa nguvu za kufanya kazi.

Katika nchi zilizoendelea kama Uingereza na Marekani, suala la uzee linahusishwa na umri wa kustaafu ambao ni miaka 65. Katika nchi nyingine umri wa kustaafu unatofautiana kijinsi, kwa mfano, nchini Latvia wanaume wanastaafu wakiwa na miaka 55 wakati wanawake wanastaafu wakiwa na umri wa miaka 60.

Pamoja na ukweli kwamba watumishi walio katika Serikali na Taasisi zake wanastaafu wanapofikia miaka 60 na kwamba wazee wa vijijini na wale waliojiajiri wanakoma kufanya kazi kutokana na kuishiwa nguvu, ukweli unabaki kwamba binadamu mwenye umri wa miaka 60 anaonyesha dalili

dhahiri za kuishiwa nguvu. Sera ya Taifa ya Afya na sheria ya utumishi wa umma zinazingatia umri wa miaka 60 kuwa ni kigezo cha uzee. Kwa madhumuni ya sera hii, mzee ni mtu mwenye umri wa miaka 60 na kuendelea.

## 1.2 HALI YA WAZEE NCHINI:

Karne ya ishirini imeshuhudia ongezeko kubwa la idadi ya wazee. Kwa kadri ya takwimu zilizopo, Tanzania yenye kukadiriwa kuwa na jumla ya watu milioni 33,500,000 ina wazee wenye umri wa miaka 60 na zaidi wapatao milioni 1.4 (asilimia 4 ya watu wote). Ifikapo mwaka 2050 idadi itaongezeka kufikia milioni 8.3 (asilimia 10 ya watu wote). Katika maisha ya kila siku ya jamii wazee wanakubalika kuwa ni watoaji wa habari, ujuzi na uzoefu. Katika maisha ya kijadi wazee na vijana waligawana majukumu. Wazee walikuwa walinzi wa mila na desturi, washauri/wapatanishi, na walezi wa watoto wadogo. Vijana wenye nguvu walikuwa na jukumu la kuwahudumia wazee hao kwa kuwapatia mahitaji ya msingi ya maisha ikiwa ni pamoja na malazi, mavazi na ulinzi. Wazee wa Tanzania wako katika makundi mbalimbali. Makundi hayo ni pamoja na Wazee Wastaafu, Wakulima, Wafugaji, Wavuvi na wale wasio na ajira. Kwa ujumla hali ya wazee wa Tanzania inatawaliwa na mazingira yafuatayo:

### 1.2.1 Mmomonyoko wa maisha ya kijadi.

Kukua kwa miji na utaratibu wa watu wengi kuhama na kutafuta kazi mbali na familia zao, kumebadili sana taratibu za mahusiano katika jamii na familia na hasa wakati hakuna kipato cha kutosha kwa ajili ya kuwasaidia wale wasiojiweza katika familia. Kutokana na hali ya utandawazi, uzee sio mhimili tegemezi katika maisha ya kila siku na hivyo kizazi cha sasa hakitegemei tena wazee kama mwongozo wa maisha katika jamii. Kutokana na hali hii vijana walio wengi wapo mbali na wazee; hawaonyeshi heshima kwa wazee na mara nyingi wanawadharau.

### 1.2.2 Matunzo duni.

Kutokana na vijana wengi kuhama vijijini na kwenda mijini, wazee wamebaki wapweke na bila ulinzi. Kutokana na hali ya ongezeko la ugonjwa wa ukimwi, vijana wengi wamepoteza maisha na hivyo kuwaacha watoto bila matunzo na jukumu hilo sasa kuchukuliwa na wazee ambao hawana msaada wowote. Matunzo ya wazee wasiojiweza limekuwa tatizo kubwa, hali hii inatokana na watoto wao kutokuwa na uwezo au moyo wa kuwasaidia.

### 1.2.3 Umasikini.

Kiuchumi wazee ni miongoni mwa watu masikini zaidi katika jamii. Makundi mbalimbali ya wazee kama wakulima, wafugaji, wavuvi na wale wasiokuwa na ajira hawamo katika mfumo wowote rasmi au usio rasmi wa hifadhi ya jamii. Wazee wastaafu walio katika mpango wa hifadhi ya jamii wanakumbwa na matatizo yanayotokana na kutotosheleza kwa mafao na urasimu wa kupata huduma. Isitoshe mikakati iliyopo ya kuondoa umasikini yaihusishi makundi ya wazee yaliyotajwa hapo juu.

### 1.2.4 Magonjwa.

Watu wengi huzeeka na kuwa na afya dhaifu kutokana na maisha na matunzo duni wakati wa ujana wao. Lishe duni wakati wa utoto au kwa wanawake mimba za mara kwa mara na kazi ngumu huongeza kasi ya kuzeeka. Magonjwa ya muda mrefu/kuendelea ni jambo la kawaida kwa wazee walio wengi. Pamoja na ukweli huo huduma za afya hazipatikani kwa urahisi kwa wazee walio wengi na mara nyingi huduma hizo ni ghali. Watumishi wa afya wanaohudumia wazee hawaonyeshi mwamko na hawana mafunzo ya kutosha katika eneo hili la huduma.

### 1.2.5 Wanawake Wazee na mila zilizopitwa na wakati.

Wanawake wazee huathirika zaidi na matatizo ya uzee. Wanawake huishi kwa muda mrefu zaidi kuliko wanaume. Ndiyo maana wanawake

wazee ni wengi zaidi kuliko wanaume. Isitoshe wanawake wazee hupambana na matatizo yanayohusiana na jinsi yao. Wazee wanawake hukosa haki ya kurithi na kumiliki mali ikiwa ni pamoja na ardhi. Kwa baadhi ya maeneo wanawake wazee wamekuwa wakilaumiwa kubakwa na kuuawa kwa imani za uchawi.

### 1.2.6 Wanawake wazee wenye ulemavu.

Kutokana na utamaduni na mazingira yetu, wanawake, watu wenye ulemavu na wazee wamekuwa hawapati fursa sawa ya kushiriki katika maamuzi mbalimbali yanayohusu maendeleo na ustawi wao. Wakati wanawake wamekuwa wanabaguliwa kutokana na jinsi yao, watu wenye ulemavu hawapati fursa ya kushiriki katika kujiletea maendeleo kutokana na hali zao. Kadhalika wazee wamekuwa hawatambuliwi ipasavyo hali ambayo inasababisha kutopata haki wanayostahili kama kumiliki na kurithi mali, isitoshe wazee hao hudhuriwa kutokana na mila potofu.

### 1.2.7 Sheria zisizolinda na kuendeleza wazee.

Kutokana na kukosa ulinzi wa kisheria, Wazee wanadhulumiwa mali zao, hawapati matunzo wanayostahili, wazee wanawake wanakosa haki ya kumiliki na kurithi mali wanapofiwa na waume zao. Mfumo wa maisha ya kijamii hautoi nafasi ya ulinzi na usalama kwa wazee kama kundi maalum.

## 1.3. Sababu za kuwa na Sera ya Wazee.

Kutokana na hali na mazingira ya wazee, upo umuhimu wa kuwa na Sera ya Taifa ya Wazee itakayokuwa mwongozo katika utoaji huduma na ushiriki wa wazee katika maisha ya kila siku. Kwa hiyo, Sera ya Taifa ya Wazee inatarajiwa kutekeleza yafuatayo:

- Kuwatambua wazee kama rasilimali muhimu katika maendeleo ya Taifa letu.

- Kuwashirikisha wazee katika maamuzi muhimu yanayowahusu wao na taifa kwa ujumla.
- Kuwashirikisha wazee katika uzalishaji mali na hivyo kuondoa umasikini miongoni mwao.
- Kuboresha huduma zinazotolewa kwa wazee.
- Kutoa ulinzi wa kisheria kwa wazee kama kundi maalum.
- Kuwaelimisha vijana kuhusu masuala ya uzee na kuzeeka na kuwajengea uwezo wa kufanya maandalizi ya maisha kuelekea uzeeni.

## SURA YA PILI

## 2.0 MWELEKEO WA SERA.

### 2.1 Mwelekeo:

Sera hii inawahusu wazee walioko vijijini na mijini, pamoja na makundi maalum ya wazee kama wastaafu, wakulima, wafugaji na wavuvi. Pia sera inawahusu vijana ambao wanapaswa kufanya maandalizi ya maisha ya uzeeni.

### 2.2 Madhumuni ya jumla.

Madhumuni ya jumla ya sera ni kuhakikisha kuwa wazee wa Tanzania wanatambuliwa na kupewa fursa ya kushiriki katika mambo yanayohusu maisha ya kila siku kwa manufaa ya Watanzania wote. Aidha kuhakikisha kwamba wazee wanapata huduma zote muhimu na za msingi ambazo zitawawezesha kushiriki kwa ukamilifu katika maisha ya kila siku ya Watanzania.

### 2.3 Madhumuni mahususi.

- Kutoa nafasi kwa wazee ili watambulike kuwa ni raslimali badala ya kuonekana ni mzigo kwa familia na jamii.

- Kujenga mazingira ambayo yatamwezesha mzee kupata na kutumia huduma muhimu za kijamii ili aweze kuishi kwa usalama na heshima.

- Kutenga rasilimali za kutosha kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na ustawi wa wazee kwa kuzingatia haki, wajibu na majukumu yao.

- Kuwezesha na kuchochea uzalishaji mali katika familia ili kuziwezesha kutoa huduma za msingi kwa wazee.

- Kuanzisha na kuendeleza programu zinazotoa fursa kwa wazee kushiriki katika mipango ya kiuchumi kwa ajili ya maendeleo yao.
- Kuandaa mikakati na programu zinazolenga katika utoaji wa picha nzuri ya wazee na kupiga vita mawazo potofu yanayoambatana na ubaguzi kiumri.
- Kutunga sheria ambazo zitalinda na kuendeleza ustawi wa wazee.
- Kuhakikisha kuwa wazee wanapata huduma za afya ya msingi.
- Kuanzisha na kuendeleza programu zinazoelimisha vijana kuhusu masuala ya uzee na kuzeeka na kuwajengea uwezo wa kufanya maandalizi ya maisha kuelekea uzeeni.
- Kuandaa programu itakayotoa fursa kwa wazee kuendeleza mila, desturi na maadili mema kwa vijana katika jamii.

# SURA YA TATU

## 3.0 MATAMKO YA SERA.

Serikali inatambua kwamba wazee ni rasilimali na hazina kubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Kuwapo kwa Taifa la Tanzania ni kielelezo tosha cha mchango mkubwa wa wazee walioutoa katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Pamoja na huduma za ulinzi na matunzo msisitizo utawekwa katika kuwahusisha na kuwashirikisha wazee katika mipango ya maendeleo ya Taifa. Sera ya wazee inazingatia pia haki za binadamu kama zilivyoanishwa na katiba ya Tanzania ya mwaka 1977 na kufanyiwa marekebisho mwaka 1984 na mwaka 1995. Kadhalika sera hii imezingatia Azimio la Umoja wa Mataifa Na. 46 la mwaka 1991 kuhusu haki za wazee zifuatazo:

- Kuwa na uhuru.
- Kushiriki na kushirikishwa.
- Kutunzwa.
- Kujiendeleza/kukuza utu wake.
- Kuheshimiwa.

Matamko ya Sera yafuatayo yanalenga katika kuweka mfumo wa utekelezaji utakaowezesha uboreshaji wa maisha na kuweka agenda ya uzee katika maendeleo ya Taifa letu.

## 3.1 Huduma za Afya.

Magonjwa ya mara kwa mara na ya muda mrefu, ni hali ya kawaida kwa wazee walio wengi. Hali hii inahitaji uangalizi na matunzo maalum ya kitaalam. Pamoja na ukweli huo, huduma za afya hazipatikani kwa urahisi kwa wazee walio wengi na mara nyingi ni ghali. Utaratibu wa kutoa huduma bure kwa wazee bado una mapungufu. Wazee walio wengi hasa wa vijijini

wanaachwa nje ya utaratibu wa kupata huduma kutokana na kushindwa kuthibitisha kwamba wana umri wa miaka 60 na hawana uwezo wa kuchangia gharama hizo. Ili kuboresha hali ya afya ya wazee Serikali kwa kushirikiana na wadau itahakikisha kwamba:-

(i) Sera ya kuchangia gharama za afya inafanyiwa mapitio kwa lengo la kufanya marekebisho ya vigezo vya utambuzi wa umri wa miaka 60.

(ii) Watumishi wa afya wanapewa mafunzo maalum ya namna ya kuwahudumia wazee.

(iii) Unawekwa utaratibu wa kufuatilia afya za wazee katika jamii.

(iv) Unawekwa utaratibu wa kuhamasisha na kuwashauri wazee kuhusu tatizo la ukimwi na matunzo ya walioathirika.

(v) Wazee na wananchi kwa ujumla watahamasishwa kuhusu matatizo ya kiafya yanayotokana na uzee kupitia njia mbalimbali.

## 3.2 Matunzo ya wazee.

Wazee ni miongoni mwa wananchi katika jamii ambao uwezo wao wa kujimudu kimaisha umepungua au haupo kabisa. Kutokana na hali hiyo jamii husika inawajibika kutoa matunzo kwa kwao hata hivyo familia bado itaendelea kuwa taasisi ya msingi katika kutoa matunzo ya wazee. Matunzo ya wazee katika makazi litakuwa ni kimbilio la mwisho baada ya njia nyingine za matunzo kushindikana. Aidha, Serikali haitarajii kuanzisha makazi mapya kwa ajili ya matunzo ya wazee. Ili kutoa matunzo kwa wazee wasio na ndugu:

(i) Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya na Wakala za Hiari itaendelea kutoa matunzo katika makazi kwa wazee na wananchi wengine ambao hawana mtu wa kuwatunza.

(ii) Matunzo kwa wazee yatatolewa kwenye jamii husika.

(iii) Familia na jamii zitaelimishwa kuhusu wajibu wao wa kuwatunza wazee.

## 3.3 Ushirikishwaji wa Wazee.

Kila mwananchi ana haki sawa ya kushiriki kikamilifu katika mambo muhimu yanayomhusu yeye mwenyewe na jamii nzima. Serikali inatambua kuwa wazee ni hazina kubwa kutokana na elimu, ujuzi na uzoefu wao. Ili kurithi hazina hii:

(i) Utawekwa utaratibu utakaohakikisha wazee wanashiriki katika uandaaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika ngazi mbalimbali.

(ii) Vyama/vikundi vinavyoshughulikia maslahi ya wazee vitaendelea kutambuliwa, aidha Serikali itahamasisha uanzishwaji wa vyama na vikundi vipya.

## 3.4 Mfuko wa Wazee.

Serikali inatambua umuhimu wa wazee kama nguvukazi katika maendeleo ya nchi na katika kuondoa umasikini. Hata hivyo nguvukazi hiyo haijatumika ipasavyo kutokana na kukosa nyenzo za utekelezaji. Ili kuwezesha utumikaji wa nguvukazi hiyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaunda mfuko wa wazee (Revolving Loan Fund) kuwawezesha kukopa ili waendeshe miradi yao.

## 3.5 Uzalishaji Mali.

Wazee ni miongoni mwa watu maskini zaidi katika jamii. Pamoja na ujuzi na uzoefu walionao kama wakulima, wafugaji, wavuvi na wastaafu katika utumishi wa umma hakuna maandalizi ya kuwawezesha Wazee kuendelea kuchangia katika maendeleo yao na ya nchi kutokana na ujuzi na uzoefu walionao. Ili kurekebisha hali hii:

(i) Mzee mmoja mmoja ama katika vikundi watahamasishwa ili waweze kuanzisha miradi ya uzalishaji mali mahali walipo.

(ii) Halmashauri za Wilaya na Wakala za Hiari zitajumuisha vikundi vilivyoazishwa na wazee katika programu zilizopo za uzalishaji mali katika jamii.

## 3.6 Hifadhi ya Jamii.

Wazee wanakabiliwa na matatizo mengi yakiwemo kutokuwa na akiba ambayo itawasaidia katika maisha yao ya uzeeni. Mfumo wa hifadhi ya jamii uliopo unawahudumia wazee waliokuwa wameajiriwa katika sekta rasmi, hata hivyo viwango vya mafao wanavyopata bado havikidhi ongezeko la gharama za maisha. Wazee wanaojishughulisha na sekta isiyo rasmi kama wakulima, wavuvi na wafugaji hasa wa vijijini wanakabiliwa na hali ngumu zaidi. Ili kurekebisha hali hii:

(i) Kutawekwa taratibu zitakazohakikisha kwamba taasisi za hifadhi ya jamii zinaelekeza huduma zake katika sekta isiyo rasmi.

(ii) Halmashauri za Wilaya na Wakala za Hiari zitahamasisha wazee walio katika sekta isiyo rasmi ili wajiwekee akiba kupitia benki kata, vyama vya msingi na vyama vya kuweka na kukopa.

(iii) Familia zitahamasishwa ili zishiriki katika shughuli za kuongeza kipato katika familia.

## 3.7 Mahitaji ya msingi ya maisha uzeeni.

Maisha ya uzee yanaambatana na upungufu wa uwezo wa mwili kufanya kazi, hali ambayo inawafanya wazee wengi wa vijijini na mijini kuwa tegemezi kimaisha. Hali hii ni mbaya zaidi kwa familia ambazo uwezo wao wa kumudu maisha ni mdogo na hivyo kusababisha wazee kuishi maisha duni. Ili kukabiliana na hali hii:

(i) Halmashauri za Wilaya kwa kushirikiana na Wakala za Hiari zitafanya utambuzi wa wazee wenye mahitaji ya msingi ya maisha ya uzeeni.

(ii) Halmashauri za Wilaya na Wakala za Hiari zitaandaa taratibu za utoaji wa mahitaji ya msingi ya moja kwa moja kwa wazee.

(iii) Familia na jamii zitahamasishwa ili zishiriki katika mipango ya uzalishaji mali ili kuinua uwezo wa kuwahudumia wazee.

### 3.8 Elimu.

Karne ya 21 ni ya sayansi na teknolojia. Mabadiliko katika sayansi na teknolojia, yamesababisha mabadiliko katika mitazamo na tabia ya binadamu. Hata hivyo katika jamii nyingi duniani, bado wazee wanalo jukumu la kuelimisha jamii kupitia mila na desturi za jamii hizo. Utamaduni huu ni muhimu sana ulindwe. Wazee hawa ni muhimu pia waishi kulingana na wakati; hivyo kupata elimu kwao itakuwa ni changamoto itakayowawezesha kufanya shughuli zao za kila siku kwa ufanisi zaidi na hatimaye kuboresha maisha yao. Ili kufanikisha azma hii:

(i) Utawekwa utaratibu wa kuelimisha wazee kuhusu haki na majukumu yao katika familia na jamii.

(ii) Utawekwa utaratibu utakaohakikisha kwamba programu za elimu ya watu wazima zinashirikisha wazee.

(iii) Utawekwa utaratibu utakaohakikisha kwamba vikundi vya wazee vinavyojihusisha na uzalishaji mali vinapata mafunzo kuhusiana na shughuli zinazofanywa na vikundi hivyo.

(iv) Utawekwa utaratibu wa kulinda na kuendeleza ila, desturi na maadili kwa vijana katika jamii.

### 3.9 Wanawake Wazee na Mila zilizopitwa na wakati.

Mila na desturi katika jamii ni mwongozo wa maisha. Matendo na tabia mbali mbali katika jamii yanajengwa na mila husika. Mila nzuri ni msingi na kichocheo cha umoja na maendeleo katika jamii inayohusika, kwa mfano, mila ya ujenzi wa nyumba au kulima shamba inayofanywa na wanakijiji kumsaidia mwenzao mwenye shida kwa malipo ya chakula cha pamoja. Mila

zilizo mbaya au potofu ni kikwazo katika mahusiano na maendeleo kwa wananchi katika jamii, kwa mfano, mila ya wajane kutokuwa na haki ya kurithi mali za waume zao waliofariki au mila ya kuua wanawake wazee kwa imani za uchawi.  Ili kukabiliana na hali hii:

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaandaa programu za uelimishaji jamii kwa lengo la kukabiliana na mila hizo.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Wakala za Hiari itawatambua akina mama wazee wanaotuhumiwa kuhusiana na imani za uchawi ili waweze kupewa matunzo na ulinzi.

### 3.10 Wanawake Wazee wenye Ulemavu.

Kutokana na hali zao wanawake wazee wenye ulemavu wanaishi katika maisha duni na ushiriki wao katika kazi za jamii ni mdogo kutokana na kukosa fursa na nyenzo za kuwasaidia kuleta maendeleo.  Ili kuboresha hali ya maisha ya wanawake hao:

(i) Utawekwa utaratibu wa kuwatambua na kuwapa mahitaji ya msingi ya maisha na matunzo kadri ya mahitaji.

(ii) Utawekwa utaratibu utakaohakikisha kwamba wanajumuishwa katika miradi ya uzalishaji mali katika maeneo waliopo.

### 3.11 Sheria zisizolinda na kuendeleza maslahi ya wazee.

Kutokana na kukosa sheria inayolinda na kuendeleza wazee, maisha ya wazee yamekosa ulinzi wa kisheria.  Ili kurekebisha hali hiyo, Serikali itatunga sheria itakayolinda na kuboresha maisha ya wazee.

### 3.12 Malezi na maandalizi ya vijana kuelekea uzeeni.

Kwa ujumla suala la uzee linagusa rika zote.  Suala la uzee kwa sasa limeonekana ni mzigo katika jamii kwani wananchi wengi wanaingia katika

hatua hii ya uzee bila maandalizi. Serikali inapaswa kuelimisha jamii hususani vijana kuhusu nafasi ya wazee katika jamii na umuhimu wa vijana kufanya maandalizi ya maisha kuelekea uzeeni. Katika kutekeleza hilo:

(i) Serikali kwa kushirikiana na asasi na wakala mbalimbali itaelimisha vijana na jamii kwa ujumla juu ya hatua na matatizo mbali mbali ya uzee.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na asasi na Wakala mbalimbali itaandaa programu zinazolenga katika kuwaelimisha na kuwajengea uwezo vijana kufanya maandalizi ya maisha kuelekea uzeeni.

(iii) Kipengele cha uzee na kuzeeka kitaongezwa katika somo la uraia kuanzia shule za msingi.

### 3.13 Vyama vya kuhudumia wazee

Serikali inatambua umuhimu wa huduma zinazotolewa na taasisi na vyama vya hiari vinavyohudumia wazee. Serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi hizo na itahakikisha kwamba huduma zinazotolewa zinazingatia viwango vinavyotakiwa.

Utaratibu wa sasa wa kusajili vyama vya hiari vinavyotoa huduma kwa wazee una mapungufu makubwa kwa sababu Wizara inayohusika na usajili haina uwezo wa kukagua utendaji kazi wa wakala hizo. Ili kurekebisha kasoro hii:

(i) Serikali itaweka utaratibu unaohakikisha kwamba usajili wa vyama vya kuhudumia wazee unapitia Wizara inayohusika na huduma kwa wazee.

(ii) Serikali itahakikisha kwamba usajili wa vyama hivyo hauambatani na ruksa ya kutoa huduma na kwamba Wizara inayohusika na huduma hiyo itoe ruksa (license) ya kutoa huduma.

(iii) Serikali itasimamia na kuratibu shughuli za wakala za hiari zinazotoa huduma kwa wazee kwa lengo la kuboresha huduma hizo.

**3.14. Mabaraza ya Wazee.**

Maamuzi kuhusu mipango shirikishi ya maendeleo ya maisha ya watu yanafanywa katika ngazi za vijiji/mitaa, kata, Wilaya, Mkoa na Taifa. Wazee ni miongoni mwa wananchi ambao mchango wao ni muhimu katika maendeleo ya Taifa letu. Upo umuhimu wa kuweka utaratibu utakaohakikisha upatikanaji wa mchango wa wazee kuhusu maisha yao na ya jamii kwa ujumla. Ili kufanikisha azma hii yataundwa mabaraza ya ushauri ya wazee katika ngazi za vijiji/mitaa, kata, Wilaya, mkoa na Taifa.

**3.15. Ushirikishwaji wa Wadau.**

Serikali inatambua na kuthamini mchango unaotolewa na wakala za hiari zinazotoa huduma kwa wazee. Serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa wakala hizo kwa lengo la kuboresha maisha ya wazee.



**SURA YA NNE**

## 4.0 MGAWANYO WA MAJUKUMU.

Suala la uzee linahusisha sekta mbalimbali katika jamii. Hivyo utekelezaji wa Sera hii hauna budi kushirikisha Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Asasi, Wakala za Hiari, Familia na Vijiji. Mgawanyo wa majukumu utakuwa kama ifuatavyo:-

### 4.1 Serikali Kuu.

- Kusimamia utoaji wa huduma kwa wazee.
- Kutunga sheria inayolinda na kuboresha maisha ya wazee.
- Kuhakikisha ushiriki wa wazee katika maisha ya jamii.
- Kuhimiza Halmashauri za Wilaya, Asasi na Wakala za Hiari ili zitoe huduma kwa wazee.
- Kuelimisha jamii kuhusu masuala ya uzee, kuzeeka na ushiriki wa wazee katika maendeleo ya Taifa.
- Kuelimisha vijana na kuwajengea uwezo wa maandalizi ya maisha kuelekea uzeeni.

### 4.2 Serikali za Mitaa.

- Kufanya utambuzi wa mahitaji ya wazee katika jamii.
- Kutoa ulinzi na matunzo kwa wazee katika jamii/asasi.
- Kutoa mahitaji ya msingi ya maisha kwa wazee.
- Kuwajumuisha wazee katika mipango ya uzalishaji mali.
- Kuelimisha jamii kuhusu masuala ya uzee, kuzeeka na ushiriki wa wazee katika maendeleo ya Taifa.
- Kuelimisha vijana na kuwajengea uwezo wa maandalizi ya maisha kuelekea uzeeni.



### 4.3 Familia/Vijiji.

- Kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa na Wakala za Hiari vitatoa ulinzi na matunzo kwa wazee.
- Kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa na Wakala za Hiari, zitashiriki katika uzalishaji mali kwa lengo la kuinua kipato.
- Kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa vitafanya utambuzi na kutoa mahitaji ya msingi ya maisha kwa wazee wahitaji.

## 4.4. Wakala za Hiari.

- Kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya zitafanya utambuzi kwa lengo la kujua mahitaji ya wazee.
- Kushirikiana na Serikali za mitaa kutoa mahitaji ya msingi ya maisha kwa wazee.
- Kutoa matunzo kwa wazee katika jamii/asasi.
- Kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa zitahamasisha na kushirikisha wazee na familia zao katika mipango ya uzalishaji mali.
- Zitaelemisha jamii kuhusu masuala ya uzee na kuzeeka na ushiriki wa wazee katika maendeleo ya Taifa.
- Kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa na Wadau wengine zitaelimisha vijana na kuwajengea uwezo wa maandalizi ya maisha kuelekea uzeeni.